JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# RIPOTI YA PATO LA MKOA WA DODOMA 2022



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA




# RIPOTI YA PATO LA MKOA WA DODOMA 2022

Ofisi ya Taifa ya Takwimu.
S.L.P 2683,
64 Barabara ya Lusinde,
44104 Tambukareli, Dodoma

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
Ofisi ya Rais – TAMISEMI
S.L.P. 914
Jengo la Mkapa (Mkapa House)
Barabara ya Hospitali ya Mkoa
41185 DODOMA

OKTOBA, 2023

## MIPAKA YA KIUTAWALA YA MKOA WA DODOMA NA HALMASHAURI




*Chanzo : Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Dodoma*

Mkoa wa Dodoma una ukubwa wa kilomita za mraba 41,311 ambazo ni sawa na asilimia 4.4 ya eneo la Tanzania Bara lenye kilomita za mraba 947,303. Aidha, katika Mkoa wa Dodoma eneo la nchi kavu ni kilomita za mraba 40,741.7 wakati kilomita za mraba 569.3 zimefunikwa na maji. Kwa taarifa hii, Mkoa wa Dodoma umechukuliwa kama eneo la kiuchumi (Economic territory) ambapo dhana ya uzalishaji wa bidhaa na huduma ilizingatiwa.

## YALIYOMO


MIPAKA YA KIUTAWALA YA MKOA WA DODOMA NA HALMASHAURI ....... i
Orodha ya Michoro ....... iii
Viambatanisho ....... iv
Dibaji ....... v
Shukrani ....... vi
1.0 Utangulizi ....... 1
2.0 Malengo ....... 1
2.1 Lengo Kuu ....... 1
2.2 Malengo Mahususi ....... 1
3.0 Manufaa ya takwimu za Pato la Mkoa ....... 1
4.0 Mawanda na Mipaka ....... 2
5.0 Methodolojia ....... 3
5.1 Mbinu za Ukokotoaji wa Pato la Mkoa ....... 3
5.1.1 Kutumia Takwimu za Uzalishaji katika ngazi ya Halmashauri ....... 3
5.1.2 Kutumia Takwimu za Uzalishaji kutoka ngazi ya Taifa ....... 3
5.2 Ukokotoaji wa Pato la Mkoa ....... 3
6.0 Matokeo Muhimu ....... 4
6.1 Pato la Mkoa ....... 4
6.2 Wastani wa Pato la Mwananchi ....... 4
6.3 Mchango katika Pato la Mkoa ....... 5
6.4 Mchango wa Makundi Makuu ya Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Mkoa Dodoma, 2022 ....... 6
7.0 Changamoto na Maazimio ....... 8
7.1 Changamoto ....... 8
7.2 Maazimio ....... 8

## ORODHA YA MICHORO

Kielelezo Na. 1 : Pato la Mkoa wa Dodoma (Shilingi Billioni) kwa Halmashauri, Mwaka 2022 ....................................... 4

Kielelezo Na. 2: Wastani wa Pato la Mwananchi kwa Halmashauri, Mkoa wa Dodoma Mwaka 2022............................ 5

Kielelezo Na. 3: Mchango wa Halmashauri katika Pato la Mkoa, Mwaka 2022 ............................................................ 5

Kielelezo Na. 4: Mchango wa Makundi Makuu ya Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Mkoa Dodoma, 2022 .............. 6

Kielelezo Na. 5: Mchango wa Sekta ya Kilimo kwa Halmashauri, 2022......................................................................... 6

Kielelezo Na. 6: Mchango wa Sekta ya Viwanda kwa Halmashauri, 2022...................................................................... 7

Kielelezo Na.7: Mchango wa sekta ya Huduma kwa Halmashauri, 2022 ...................................................................... 7

## VIAMBATANISHO

Kiambatisho Na 1: Dhana na Ufafanuzi ........ 9

Kiambatisho Na 2: Majedwali ........ 11

Jedwali la 1: Pato la Mkoa wa Dodoma kwa Halmashauri, 2018 - 2022 ........ 11

Jedwali la 1: Idadi ya Watu kwa Mkoa wa Dodoma kwa Halmashauri, 2018 - 2022 ........ 11

Jedwali la 2: Wastani wa Pato la Mwananchi kwa Halmashauri, 2018 – 2022 ........ 11

Jedwali la 4: Pato la Mkoa wa Dodoma kwa shughuli za kiuchumi, Bei za Miaka husika, 2018 - 2022 ........ 12

Jedwali la 5: Pato la Mkoa kwa shughuli za kiuchumi kwa Halmashauri, (Bei ya Mwaka Husika), 2018 ........ 13

Jedwali la 6: Pato la Mkoa kwa shughuli za kiuchumi kwa Halmashauri, (Bei ya Mwaka Husika), 2019 ........ 14

Jedwali la 7: Pato la Mkoa kwa shughuli za kiuchumi kwa Halmashauri, (Bei ya Mwaka Husika), 2020 ........ 15

Jedwali la 8: Pato la Mkoa kwa shughuliza kiuchumi kwa Halmashauri, (Bei ya Mwaka Husika), 2021 ........ 16

Jedwali la 9: Pato la Mkoa kwa shughuliza kiuchumi kwa Halmashauri, (Bei ya Mwaka Husika), 2022 ........ 17

Jedwali la 10: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi kwa Halmashauri kwa Bei ya Mwaka Husika kwa , 2022 ........ 18

Jedwali la 11: Vyanzo vya Taarifa zilizotumika kutayarisha Pato la Mkoa kwa kila Shughuli ya kiuchumi ........ 19

## DIBAJI

Pato la Mkoa wa Dodoma linapima thamani ya bidhaa na huduma zilizozalishwa katika kipindi cha mwaka mmoja na pia inaonesha mwenendo wa ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika mkoa kati ya mwaka mmoja na mwingine. Pato la Mkoa wa Dodoma ni kiashiria muhimu cha kiuchumi ambacho kitatumika katika kupanga na kuratibu maendeleo ya mkoa. Kwa mwaka 2022, Pato la Mkoa wa Dodoma lilikuwa shilingi milioni 5,418,844 ambapo sekta ya Kilimo ilichangia asilimia 39.8, Viwanda na Ujenzi asilimia 28.0, na Huduma asilimia 32.2 katika Pato la Mkoa. Aidha, Halmashauri ya Jiji la Dodoma imeongoza kwa kuchangia asilimia 33.5 katika Pato la Mkoa wakati Halmashauri ya Wilaya ya Chemba imechangia kwa kiwango kidogo cha asilimia 5.9 katika Pato la Mkoa.

Aidha, taarifa hii inaonesha wastani wa pato kwa kila mwananchi wa mkoa wa Dodoma na pia wastani wa pato kwa kila mwananchi kwa halmashauri.

Utayarishaji wa Pato la Mkoa wa Dodoma umezingatia kanuni na mwongozo unaotolewa na Umoja wa Mataifa chini ya Kitengo cha Takwimu cha Kutayarisha Takwimu za Pato la Taifa hususan chapisho la mwaka 2008 yaani "*United Nation System of National Accounts* (2008 SNA)". Matumizi ya mwongozo huo yanawezesha nchi kutayarisha na kulinganisha takwimu za Pato la Taifa la nchi moja na nyinginezo duniani kwa kuwa mfumo wa utayarishaji ni uleule.

Matayarisho ya Pato la Mkoa wa Dodoma yamegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni ngazi ya Mkoa na Halmashauri. Taarifa ya Pato la Mkoa wa Dodoma imetayarishwa mwaka 2022 ikijumuisha taarifa za miaka mitano kuanzia 2018 – 2022, kwa kutumia bei za miaka husika. Aidha, Pato la Mkoa ni kanzidata ya taarifa ya kiuchumi ya mkoa ambayo pia itatumika kama rejea katika kutayarisha Pato la Mkoa wa Dodoma kwa miaka ijayo. Taarifa hii inahitimisha kazi ya pamoja kati ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

Katika kukamilisha taarifa ya Pato la Mkoa wa Dodoma, Wataalam kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa walisimamia na kufanikisha ukusanyaji wa taarifa za uzalishaji wa bidhaa na huduma kutoka katika shughuli mbalimbali za kiuchumi katika mkoa wa Dodoma. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilitoa wataalam mahiri katika kutayarisha Takwimu za Pato la Taifa, waliosimamia utayarishaji wa Pato la Mkoa wa Dodoma. Methodolojia iliyotumika inakubalika kimataifa.

Pato la Mkoa wa Dodoma limetayarishwa kwa lengo la kutoa taarifa muhimu za kiuchumi kwa Serikali na kwa wadau mbalimbali zinazoakisi shughuli za kiuchumi katika mkoa. Taarifa hii imeelezea changamoto zilizojitokeza wakati wa zoezi la utayarishaji wa Pato la Mkoa wa Dodoma. Changamoto hizo zitatafutiwa ufumbuzi na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ikishirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa lengo la kuboresha taarifa za uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa ajili ya utayatishaji wa Pato la Mkoa wa Dodoma kwa miaka ijayo. Ni matarajio yangu kwamba, taarifa hii itakuwa nyenzo muhimu ya rejea katika kupanga na kutayarisha shughuli za maendeleo ya kiuchumi ya Mkoa.

**Dkt. Albina Chuwa**
Mtakwimu Mkuu wa Serikali
Ofisi ya Taifa ya Takwimu
S.L.P 2683, Dodoma
Simu: +255 26 2963822
Nukushi: +255 26 2963828

Ofisi ya Taifa ya Takwimu inakaribisha maoni kuhusu chapisho hili. Maoni haya yapelekwe kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

Taarifa zaidi za Takwimu za Pato la Taifa zinapatikana kupitia tovuti ifuatayo: www.nbs.go.tz

## SHUKRANI

Utayarishaji wa taarifa ya Pato la Mkoa wa Dodoma uliwezekana kwa juhudi za pamoja za Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Halmashauri za Mkoa wa Dodoma. Kazi hiyo iliongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma chini ya uratibu wa Katibu Tawala wa Mkoa, Ndugu Ally Senga Gugu, Katibu Tawala Msaidizi - Mipango na Uratibu, Bw. Charles A. Mduma, Mtakwimu wa Mkoa Bi Josephine P. Nyengela na Meneja wa Takwimu Mkoa Bw. Idd A. Muruke waliosimamia mchakato mzima wa ukusanyaji takwimu.

Napenda kuwashukuru Wakurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Halmashauri ya Mji wa Kondoa, na Halmashauri za wilaya ya Mpwapwa, Kongwa, Chamwino, Bahi na Chemba pamoja na viongozi wengine wa Halmashauri walioratibu ukusanyaji wa takwimu. Aidha, nawashukuru wananchi, Taasisi za Umma na Sekta Binafsi kwa ushirikiano wao katika utoaji wa takwimu zilizotumika katika kutayarisha Pato la Mkoa.

Vilevile,namshukuru Mtakwimu Mkuu wa Serikali, pamoja na wataalam wake wakiongozwa na Mkurugezi wa Takwimu za Uchumi, Bw. Daniel Masolwa, Meneja wa Takwimu za Pato la Taifa, Bi. Adella Ndesangia na wataalam wengine ambao ni Bw. Ernest E. Mshana na Bw. Boniface Simpoli Yohana kwa michango yao katika kutayarisha taarifa hii muhimu.



**Mhe. Rosemary Staki Senyamule**
**Mkuu wa Mkoa wa Dodoma**
**S.L.P 914**
**POSTIKODI: 41185 DODOMA**
**Simu: +255: (026) 2324343/2324384**
**Nukushi: +255: (026) 2320046**
**Baruapepe: ras@dodoma.go.tz,**
**Tovuti: www.dodoma.go.tz**

# 1.0 Utangulizi

Taarifa ya Pato la Mkoa wa Dodoma ni matokeo ya kazi ya pamoja kati ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma. Mchakato wa kuandaa taarifa hii ulianza mwezi Mei 2023 kwa kutoa mafunzo kuhusu mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za kitakwimu na kuandaa ratiba ya kazi ya utayarishaji wa takwimu za Pato la Mkoa.

Mpangilio wa kazi ulikuwa kama ifuatavyo:

- Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ilikuwa na jukumu la kuratibu na kusimamia zoezi la ukusanyaji wa taarifa za uzalishaji wa bidhaa na huduma katika Mkoa; na
- Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilikuwa na jukumu la kutayarisha madodoso na mwongozo kwa ajili ya ukusanyaji wa taarifa za kitakwimu na kuandaa sampuli pamoja na kutoa utaalamu kuhusu ukokotoaji wa takwimu za Pato la Mkoa.

# 2.0 Malengo

## 2.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la kutayarisha taarifa ya Pato la Mkoa wa Dodoma ni kutoa viashiria muhimu vya kiuchumi ambavyo vitatumika katika kupanga mipango ya maendeleo ya Mkoa. Aidha, taarifa ya Pato la Mkoa wa Dodoma itatumika katika kuboresha sera na mipango ya Mkoa na Halmashauri. Vilevile, Serikali itatumia taarifa hii kutathimini maendeleo ya kiuchumi ya Mkoa wa Dodoma.

## 2.2 Malengo Mahususi

Malengo mahususi ya kutayarisha taarifa ya Pato la Mkoa wa Dodoma yalikuwa:-

a) Kukusanya, Kukokotoa na kutafsiri Pato la Mkoa wa Dodoma kwa aina ya shughuli za kiuchumi ambazo zimeainishwa kwa kila Halmashauri; na
b) Kukokotoa wastani wa pato la kila mwananchi katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri.

# 3.0 Manufaa ya takwimu za Pato la Mkoa

Takwimu za Pato la Mkoa hutoa taarifa muhimu kwa ajili ya kupanga mipango ya maendeleo ya Mkoa kwa kuwa

a) Husaidia kupata uelewa zaidi wa ukuaji wa uchumi na utendaji wa mkoa;
b) Hutoa msingi wa ufuatiliaji na tathmini ya mwenendo wa maendeleo ya uchumi;
c) Hutumiwa na Serikali Kuu katika kupanga mipango ya maendeleo ya mkoa, ikijumuisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP) na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri;
d) Hutumika katika kuweka misingi imara ya kufanya maamuzi ya kiuchumi kwa mkoa, wilaya na sekta binafsi;
e) Ni msingi wa taarifa muhimu kwa ajili ya mijadala ya umma na uelewa wa jamii juu ya maendeleo ya uchumi wa mkoa;
f) Hutoa takwimu za msingi zitakazosaidia kushughulikia masuala muhimu kama vile kupunguza umaskini na kukuza viwanda kwa mfano usindikaji wa mazao ya kilimo;
g) Hutumika katika ugawaji wa rasilimali na uwekezaji katika ngazi ya mkoa na wilaya; na
h) Huonesha fursa za kiuchumi zinazopatikana katika mkoa na halmashauri zake ambazo zinaweza kuvutia wawekezaji wa sekta mbalimbali katika mkoa.

## 4.0 Mawanda na Mipaka

Mipaka ya Mkoa na Halmashauri imechukuliwa kama eneo la kiuchumi (economic teritory) katika kutayarisha taarifa ya Pato la Mkoa na Halmashauri ambapo miamala (transactions) ya bidhaa na huduma hufanyika, ikihusisha mawanda ya shughuli zote za kiuchumi.

Taarifa ya Pato la Mkoa wa Dodoma imeandaliwa kutokana na shughuli za kiuchumi ambazo zimeainishwa kwa kuzingatia mfumo wa kimataifa wa ukokotoaji wa takwimu za Pato la Taifa. Mfumo huohuo umetumika kukokotoa takwimu za Pato la mkoa wa Dodoma. Aina ya shughuli za kiuchumi zilizoainishwa katika kutayarisha Pato la Mkoa ni:

a) Kilimo;
    i. Mazao;
    ii. Mifugo;
    iii. Misitu na Uwindaji;
    iv. Uvuvi;
b) Uchimbaji wa Madini na Mawe;
c) Utengenezaji bidhaa;
d) Uzalishaji, Usambazaji na Ugavi wa Umeme;
e) Maji safi na maji taka;
f) Ujenzi;
g) Biashara na Matengenezo;
h) Usafirishaji na Uhifadhi mizigo;
i) Huduma za Malazi na Chakula;
j) Habari na Mawasiliano;
k) Fedha na Bima;
l) Upangishaji Majengo;
m) Shughuli za Kitaalamu, Sayansi na Ufundi;
n) Huduma za Kiutawala;
o) Utawala na Ulinzi;
p) Elimu;
q) Afya na Huduma za Jamii;
r) Sanaa na Burudani; na
s) Huduma nyingine.

Kwa kuzingatia Mfumo wa Kimataifa wa Kukokotoa Pato Taifa (2008 SNA) shughuli tajwa hapo juu zimegawanyika katika makundi makuu matatu ambayo ni:

i. Kilimo (Mazao, Mifugo, Misitu na Uvuvi);
ii. Viwanda na Ujenzi (Uchimbaji madini na mawe, Utengenezaji bidhaa viwandani, Umeme, Maji safi na maji taka na Ujenzi); na
iii. Huduma (Biashara ya jumla na reja reja na Matengenezo, Huduma za Malazi na Chakula, Usafirishaji na Uhifadhi mizigo, Habari na Mawasiliano, Fedha na Bima, Upangishaji Majengo, Shughuli za kitaaluma, kisayansi na kiufundi, Huduma za Kiutawala, Utawala na Ulinzi, Elimu, Afya na Huduma za Jamii, Sanaa na Burudani na Huduma Nyingine za kijamii na kibinafsi).

Kwa kiasi kikubwa uchumi wa Mkoa wa Dodoma unategemea kilimo, hususan kilimo cha mazao ya chakula na biashara. Mazao yanayozalishwa kwa wingi katika Mkoa huu ni pamoja na mahindi, mtama, uwele, mpunga, alizeti na zabibu.

## 5.0 Methodolojia

### 5.1 Mbinu za Ukokotoaji wa Pato la Mkoa

Mbinu zilizotumika kukokotoa Pato la Mkoa zilizingatia Mwongozo unaotolewa na Umoja wa Mataifa chini ya Kitengo cha Takwimu cha Kutayarisha Takwimu za Pato la Taifa hususan chapisho la mwaka 2008 yaani "United Nation System of National Accounts (*2008 SNA*)". Aidha, Pato la Mkoa lilipimwa kutokana na thamani ya bidhaa na huduma zilizozalishwa ukiondoa gharama za uzalishaji ukijumlisha kodi na kutoa ruzuku iliyotumika katika uzalishaji. Mbinu zilizotumika kukokotoa Pato la Mkoa ni:-

#### 5.1.1 Kutumia Takwimu za Uzalishaji katika ngazi ya Halmashauri

Kwa kutumia mbinu hii, Pato la Mkoa lilitayarishwa kwa kutumia taarifa za uzalishaji wa bidhaa na huduma zilizokusanywa kutoka ngazi ya Halmashauri (*Botton - up Approach*). Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ilisimamia zoezi la ukusanyaji wa taarifa za uzalishaji wa bidhaa na huduma zilizotumika katika kukokotoa Pato la Mkoa.

#### 5.1.2 Kutumia Takwimu za Uzalishaji kutoka ngazi ya Taifa

Mbinu ya kutumia takwimu za uzalishaji kutoka ngazi ya taifa (*Top - down Approach*), inatumika iwapo taarifa za kina za uzalishaji wa bidhaa na huduma zilizokusanywa katika ngazi za halmashauri hazijitoshelezi Mbinu hii inahusisha kugawanya Pato la Taifa kwenye mikoa kwa kutumia viashiria mbalimbali vilivyoainishwa kwa aina ya shughuli za kiuchumi ili kupata Pato la Mkoa husika.

### 5.2 Ukokotoaji wa Pato la Mkoa

Kuna njia tatu za ukokotoaji wa Pato la Mkoa ambazo ni Uzalishaji, Mapato na Matumizi. Kwa kawaida thamani ya Pato la Mkoa kwa kutumia njia zote inatakiwa kuwa sawa.

Pato la Mkoa kwa njia ya uzalishaji (Production *Approach*) ni thamani ya bidhaa na huduma zilizozalishwa ukiondoa gharama za kati (intermediate consumption) zilizotumika katika kuzalisha bidhaa na huduma kwa bei za mwaka husika, ikijumuisha kodi na kutoa ruzuku iliyotumika katika uzalishaji.

Pato la Mkoa kwa njia ya mapato (Income Approach) inajumuisha mishahara ya wafanyakazi thamani ya kupungua kwa rasilimali za kudumu zinazotumika katika uzalishaji wa bidhaa na huduma (consumption of fixed capital); faida ya mwekezaji (operating surplus) baada ya kuondoa gharama za uzalishaji; na ruzuku na ushuru katika uzalishaji.

Pato la Mkoa kwa njia Matumizi (*Expenditure Approach*) linajumuisha matumizi ya mwisho ya serikali; Kaya binafsi na Asasi zisizo za Kiserikali zinazohudumia kaya binafsi; Ukuzaji wa rasilimali; thamani ya bidhaa na huduma zilizouzwa nje ya mkoa na thamani ya bidhaa na huduma zilizonunuliwa toka nje ya mkoa.

Njia ya uzalishaji wa bidhaa ilitumika katika kutayarisha Pato la Mkoa wa Dodoma kwa kuwa taarifa za uzalishaji wa bidhaa ni za kuaminika zaidi ikilinganishwa na njia ya Mapato au njia ya Matumizi. Changamoto ya kutumia njia ya matumizi inatokana na kutokuwepo kwa ofisi za forodha kati ya mkoa mmoja na mwingine, hivyo kutopatikana kwa taarifa za uagizaji na uuzaji wa bidhaa kati ya mkoa mmoja na mwingine. Aidha, changamoto ya kutumia njia ya mapato ni kutokuwepo kwa taarifa za kupungua kwa rasilimali za kudumu zinazotumika katika uzalishaji wa bidhaa na huduma.

Pato la Mkoa wa Dodoma limetayarishwa katika ngazi ya Halmashauri za Mkoa wa Dodoma ambapo Pato la Halmashauri zote likijumishwa pamoja unapata Pato la Mkoa wa Dodoma.


## 6.0 Matokeo Muhimu

Pato la Mkoa wa Dodoma limetayarishwa kwa kuzingatia mipaka ya Halmashauri, ambapo takwimu za wastani wa pato la kila mwanachi katika Mkoa wa Dodoma pamoja na mchango wa shughuli za kiuchumi katika Pato la Mkoa vimebainishwa.

### 6.1 Pato la Mkoa

Mwaka 2022, Pato la Mkoa wa Dodoma kwa Bei za Soko lilikuwa na thamani ya Shilingi Bilioni 5,418.9. Aidha, Halmashauri ya Jiji la Dodoma ilikuwa na Pato la juu zaidi kuliko halmashauri zote la Shilingi Bilioni 1,814 wakati Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ikiwa na Pato la chini zaidi katika Mkoa la Shilingi Bilioni 318 ( Kielelezo Na. 1). Katika kipindi cha kati ya mwaka 2018 – 2022, Pato la Mkoa wa Dodoma liliongezeka kwa shilingi bilioni 1,675,829. Ongezeko kubwa lilikuwa kati ya mwaka 2019 na 2020 ambalo lilikuwa shilingi bilioni 714,187, wakati ongezeko dogo lilikuwa kati ya mwaka 2020 na 2021 la shilingi bilioni 269,505.


**Kielelezo Na. 1 : Pato la Mkoa wa Dodoma (Shilingi Billioni) kwa Halmashauri, Mwaka 2022**




### 6.2 Wastani wa Pato la Mwananchi

Wastani wa pato la mwananchi kwa bei ya soko kwa mkoa wa Dodoma ulikuwa Shilingi 1,756,158 kwa mwaka 2022, ambao upo chini ya wastani wa pato la Taifa kwa kila mwananchi wa Shilingi 2,577,967. Hata hivyo, Halmashauri ya Mji wa Kondoa ilikuwa na wastani wa pato la mwananchi wa Shilingi 4,349,474 ambao ni zaidi ya wastani wa pato la mwananchi la Mkoa wa Dodoma na pia wastani wa pato la Taifa kwa kila mwananchi. Aidha, mwaka 2022, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ilikuwa na wastani wa pato la mwananchi wa Shilingi 935,832 ambao ni wa chini zaidi ukilinganishwa na Halmashuri nyingine za Mkoa wa Dodoma (Kielelezo Na. 2).


**Kielelezo Na. 2: Wastani wa Pato la Mwananchi kwa Halmashauri, Mkoa wa Dodoma Mwaka 2022**




### 6.3 Mchango katika Pato la Mkoa

Mwaka 2022, mchango wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwenye Pato la Mkoa ulikuwa mkubwa kwa asilimia 33.5 ikilinganishwa na Halmashauri nyingine za Mkoa wa Dodoma. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ilikuwa na mchango mdogo wa asilimia 5.9 kwenye Pato la Mkoa (Kielelezo Na. 3).


**Kielelezo Na. 3: Mchango wa Halmashauri katika Pato la Mkoa, Mwaka 2022**



## 6.4 Mchango wa Makundi Makuu ya Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Mkoa Dodoma, 2022


Uchambuzi wa shughuli za kiuchumi kwa makundi makuu, kama ilivyoainishwa kwenye 2008 SNA, umeonesha kuwa Sekta ya Kilimo katika Pato la Mkoa ilikuwa na mchango mkubwa zaidi wa asilimia 39.8, ikifuatiwa na mchango wa Sekta ya Huduma wa asilimia 32.2 na Sekta ya Viwanda na Ujenzi ilikuwa na mchango wa asilimia 28.0 (Kielelezo Na. 4).

**Kielelezo Na. 4: Mchango wa Makundi Makuu ya Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Mkoa Dodoma, 2022**





Shughuli za Kilimo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa zilichangia kwa kiwango kikubwa cha asilimia 7.5 katika pato la Mkoa. Aidha shughuli za kilimo katika Halmashauri ya mji wa Kondoa zilichangia kiwango kidogo cha asilimia 0.6 katika pato la Mkoa kwa mwaka 2022 (Kielelezo Na. 5).

**Kielelezo Na. 5: Mchango wa Sekta ya Kilimo kwa Halmashauri, 2022**




Shughuli za Viwanda na Ujenzi katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma zilichangia kwa kiwango kikubwa cha asilimia 13.4 katika pato la Mkoa. Aidha shughuli za Viwanda na Ujenzi katika Halmashauri ya wilaya ya Chemba zilichangia kiwango kidogo cha asilimia 0.7 katika pato la Mkoa kwa mwaka 2022 (Kielelezo Na. 6).

**Kielelezo Na. 6: Mchango wa Sekta ya Viwanda na Ujenzi kwa Halmashauri, 2022**




Shughuli za Huduma katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma zilichangia kwa kiwango kikubwa cha asilimia 14.5 katika pato la Mkoa. Aidha shughuli za Huduma katika Halmashauri ya wilaya ya Kondoa zilichangia kiwango kidogo cha asilimia 1.6 katika pato la Mkoa kwa mwaka 2022 (Kielelezo Na. 7).

**Kielelezo Na.7: Mchango wa sekta ya Huduma kwa Halmashauri, 2022**



## 7.0 Changamoto na Maazimio

### 7.1 Changamoto

Miongoni mwa changamoto zilizojitokeza wakati wa utayarishaji wa taarifa ya Pato la Mkoa wa Dodoma ni pamoja na:-

- Kukosekana kwa baadhi ya takwimu muhimu za uzalishaji wa bidhaa na huduma pamoja na taarifa za mapato na matumizi katika mizania (Balance Sheet) za Taasisi;
- Uelewa mdogo juu ya umuhimu wa kuhifadhi taarifa za kitakwimu kwa baadhi ya wahojiwa; na
- Ugumu wa utoaji wa taarifa za kitakwimu, kwa baadhi ya wahojiwa wakidhani kwamba takwimu hizo zitatumika kwa ajili ya kutoza kodi.

### 7.2 Maazimio

Kutokana na changamoto zilizojitokeza, maeneo yafuatayo yanapendekezwa kuboreshwa katika utayarishaji wa Pato la Mkoa kwa wakati ujao.

- Kwa kuwa taarifa hii ya Pato la Mkoa wa Dodoma ni ya kwanza tangu Jiji la Dodoma lilipotangazwa kuwa Makao Makuu ya Serikali, inapendekezwa kuendelea kutayarisha takwimu za Pato la Mkoa kwa miaka ijayo ili kupata mwenendo na ukuaji wa uchumi wa Mkoa wa Dodoma;
- Takwimu za Pato la Mkoa ziwasilishwe kwa wadau mbalimbali ili kuweza kupata maoni yao kwa ajili ya kuboresha taarifa ya Pato la Mkoa;
- Kuanzisha makubaliano (Memorundum Of Understanding) mahususi kati ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu ili kuhakikisha kuwa takwimu kwa ajili ya kutayarisha Pato la Mkoa zinapatikana kwa wakati na kwa ubora unaohitajika;
- Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ikishirikiana na Oisi ya Taifa ya Takwimu zianzishe programu ya makusudi ya mafunzo kwa waratibu na wakusanyaji wa taarifa ngazi ya Mkoa na Halmashauri ili kuhakikisha ubora wa takwimu kwa ajili ya kutayarisha Pato la Mkoa;
- Kuendelea kuhamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa ukusanyaji na utoaji wa taarifa sahihi kwa wakati; na
- Kuwepo na bajeti mahususi katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Halmashauri kwa ajili ya utayarishaji wa Pato la Mkoa.

## Kiambatisho Na 1: Dhana na Ufafanuzi

Maana ya Maelezo yanayotumika katika Taarifa ya Pato la Taifa

**Bei ya Mzalishaji *(Basic Price)***

Kiasi cha mapato kilichopokelewa na mzalishaji kutoka kwa mnunuzi kwa mauzo ya bidhaa au huduma inayozalishwa, ukiondoa kodi yoyote inayolipwa na kuongeza ruzuku yoyote inayopatikana. Pia, ukiondoa gharama zozote za usafiri zilizogharamiwa na mzalishaji.

**Mishahara kwa Wafanyakazi**

Hii ni jumla ya malipo anayolipwa mwajiriwa kutoka kwa mwajiri kwa fedha taslimu au malipo kwa huduma. Mishahara inajumuisha michango inayolipwa kwenye mifuko ya pensheni ikiwa ni fedha za malipo ya uzeeni, bima, fidia na marupurupu mengine.

**Kupungua kwa Thamani ya Rasilimali ya Kudumu**

Ni kupungua kwa thamani ya rasilimali ya kudumu kutokana na kutumika katika uzalishaji kwa kipindi cha mwaka. Kupungua kwa thamani kunasababishwa na kuchakaa kwa kawaida au uharibifu wa bahati mbaya na inathaminiwa kwa gharama ya kununua nyingine.

**Pato la Taifa**

Jumla ya ongezeko la thamani ya bidhaa na huduma zinazozalishwa katika eneo la kiuchumi ikiwa ni pamoja na kodi ukiondoa ruzuku iliyotumika wakati wa uzalishaji.

**Pato la Taifa kwa Bei za Soko**

Pato la Taifa linalojumuisha gharama za usafirishaji wa bidhaa hadi sokoni, kodi na ushuru uliotozwa na kuondoa ruzuku iliyotolewa wakati wa uzalishaji wa bidhaa.

**Pato la Taifa kwa Bei ya Mwaka wa Kizio**

Pato la Taifa (GDP) kwa bei ya mwaka wa rejea (kizio) ambayo hutumika kupima ukuaji halisi wa shughuli za kiuchumi kati ya mwaka mmoja na mwingine.

**Salio la Uendeshaji (Faida ya Mwezeshaji)**

Jumla ya thamani ya bakaa (salio) ya uzalishaji wa bidhaa na huduma baada ya kutoa matumizi ya uzalishaji kama vile matumizi ya kati, kodi, ruzuku ya uzalishaji na uagizaji.

**Matumizi ya Kati**

Ni thamani ya bidhaa na huduma, zisizo za kudumu, zinazotumiwa katika uzalishaji na inathaminishwa kwa kutumia bei ya mnunuzi. Matumizi ya kati hayajumuishi malipo ya mishahara au kupungua kwa thamani ya rasilimali za kudumu zilizotumika katika uzalishaji wa bidhaa.

**Pato Ghafi**

Ni jumla ya thamani ya uzalishaji wa bidhaa na huduma iliyopatikana ndani ya taasisi ambayo inaweza kutumiwa na taasisi nyingine. Aidha, thamani ya uzalishaji wa bidhaa inajumuisha pia bidhaa kwa ajili ya matumizi ya taasisi husika.

**Thamani ya Mzalishaji**

Thamani ya bidhaa na huduma kwa bei ya soko ukiondoa gharama ya usafirishaji pamoja na gharama zingine zilizolipwa kwa bidhaa kufika sokoni. Hii inatoa thamani ya mauzo ya soko kwa mzalishaji kwenye kiwanda, shamba, au mgodi. Kwa shughuli za huduma, thamani ya mzalishaji ni sawa na thamani ya mnunuzi, kwa kuwa Huduma zinazalishwa na kutumiwa kwa wakati mmoja.

**Thamani ya Mnunuzi**

Ni gharama katika soko la bidhaa na huduma anazogharamia mnunuzi. Kwa shughuli za huduma, thamani ya mnunuzi ni sawa na thamani ya mzalishaji, kwa kuwa huduma zinazalishwa na kutumiwa kwa wakati mmoja.

**Ruzuku**

Malipo yaliyofanywa na Serikali kwa taasisi, yasiyorejeshwa, kwa ajili ya kufidia baadhi ya gharama zilizotumika katika kuzalisha bidhaa na huduma kwa mlaji, kuuza ndani au nje ya nchi.

**Ushuru wa Uzalishaji na Uagizaji**

Kodi zinazotozwa kwa wazalishaji kuhusiana na uzalishaji, uuzaji, ununuzi na matumizi ya bidhaa na huduma, ambazo zinajumuishwa katika bei ya soko ya bidhaa na huduma hizo. Hii ni pamoja na kodi ya mauzo, kodi ya serikali ya mitaa, ushuru wa kuagiza bidhaa, ada ya usajili inayolipwa na wazalishaji.

**Ongezeko la Thamani**

Thamani iliyoongezeka kwenye bidhaa na huduma kwa kutumia mtaji  na nguvukazi baada ya kutoa gharama ya uzalishaji.

**Taasisi**

Ni kaya au kikundi kinachofanya biashara katika eneo moja na inazalisha aina moja tu ya bidhaa.

## Kiambatisho Na 2: Majedwali

**Jedwali la 1: Pato la Mkoa wa Dodoma kwa Halmashauri, 2018 – 2022**

..........................................................................................................................................................**Sh. Milioni**

| Halmashauri | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kondoa | 439,511 | 456,099 | 515,873 | 524,732 | 537,040 |
| Mpwapwa | 343,183 | 410,351 | 405,915 | 460,260 | 465,600 |
| Kongwa | 401,620 | 467,609 | 665,355 | 613,155 | 671,188 |
| Chamwino | 315,411 | 344,421 | 387,858 | 524,260 | 560,361 |
| Dodoma Jiji | 1,235,953 | 1,345,460 | 1,491,216 | 1,621,803 | 1,814,020 |
| Bahi | 522,450 | 463,508 | 677,698 | 629,566 | 703,191 |
| Chemba | 241,618 | 266,414 | 293,739 | 302,711 | 317,559 |
| Kondoa Mji | 243,269 | 285,227 | 315,621 | 346,294 | 349,885 |
| Pato la Mkoa | 3,743,015 | 4,039,088 | 4,753,275 | 5,022,780 | 5,418,844 |

**Chanzo:** NBS na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

**Jedwali la 1: Idadi ya Watu kwa Mkoa wa Dodoma kwa Halmashauri, 2018 - 2022**

| Halmashauri | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kondoa | 241,897 | 250,307 | 259,111 | 268,311 | 244,854 |
| Mpwapwa | 368,037 | 378,940 | 390,320 | 402,173 | 403,247 |
| Kongwa | 372,407 | 383,701 | 395,493 | 407,781 | 443,867 |
| Chamwino | 396,138 | 405,260 | 414,756 | 424,619 | 486,176 |
| Dodoma Jiji | 506,942 | 523,010 | 539,799 | 557,309 | 765,179 |
| Bahi | 263,780 | 271,069 | 278,669 | 286,578 | 322,526 |
| Chemba | 274,083 | 283,731 | 293,834 | 304,394 | 339,333 |
| Kondoa Mji | 69,705 | 72,496 | 75,428 | 78,504 | 80,443 |
| **Jumla** | **2,492,989** | **2,568,514** | **2,647,410** | **2,729,668** | **3,085,625** |

**Chanzo:** NBS na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

**Jedwali la 2: Wastani wa Pato la Mwananchi kwa Halmashauri, 2018 – 2022**

..........................................................................................................................................................**Shilingi**

| Halmashauri | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kondoa | 1,816,936 | 1,822,157 | 1,990,936 | 1,955,688 | 2,193,308 |
| Mpwapwa | 932,470 | 1,082,891 | 1,039,956 | 1,144,432 | 1,154,627 |
| Kongwa | 1,078,444 | 1,218,680 | 1,682,344 | 1,503,637 | 1,512,138 |
| Chamwino | 796,216 | 849,875 | 935,146 | 1,234,660 | 1,152,589 |
| Dodoma Jiji | 2,438,055 | 2,572,533 | 2,762,539 | 2,910,060 | 2,370,714 |
| Bahi | 1,980,628 | 1,709,927 | 2,431,907 | 2,196,841 | 2,180,261 |
| Chemba | 881,549 | 938,966 | 999,678 | 994,471 | 935,832 |
| Kondoa Mji | 3,489,979 | 3,934,377 | 4,184,396 | 4,411,189 | 4,349,474 |
| **Wastani wa Pato la Mkoa kwa kila Mwananchi wa Dodoma** | **1,501,417** | **1,572,539** | **1,795,444** | **1,840,070** | **1,756,158** |
| **Wastani wa Pato la Taifa kwa kila Mwananchi** | **1,968,965** | **2,191,190** | **2,327,395** | **2,452,406** | **2,577,967** |

**Chanzo:** NBS na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

**Jedwali la 4: Pato la Mkoa wa Dodoma kwa shughuli za kiuchumi, Bei za Miaka husika, 2018 - 2022**

**Shilingi. Milioni**

| Shughuli za Kiuchumi | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Kilimo** | **1,360,612** | **1,422,136** | **1,873,958** | **1,907,259** | **2,158,358** |
| Mazao | 1,149,969 | 1,184,396 | 1,626,426 | 1,636,189 | 1,857,090 |
| Mifugo | 199,275 | 225,791 | 235,103 | 257,840 | 287,868 |
| Misitu na Uwindaji | 7,140 | 8,145 | 8,892 | 8,660 | 10,164 |
| Uvuvi | 4,228 | 3,804 | 3,537 | 4,571 | 3,236 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **1,027,697** | **1,145,312** | **1,301,096** | **1,463,669** | **1,518,093** |
| Uchimbaji madini na mawe | 242,298 | 284,808 | 318,855 | 351,088 | 388,563 |
| Utengenezaji bidhaa | 313,940 | 369,635 | 404,943 | 456,771 | 463,801 |
| Umeme | 30,842 | 18,430 | 15,044 | 15,734 | 17,725 |
| Maji | 20,168 | 26,260 | 24,918 | 25,337 | 29,702 |
| Ujenzi | 420,448 | 446,180 | 537,336 | 614,739 | 618,302 |
| **Huduma** | **1,354,707** | **1,471,639** | **1,578,221** | **1,651,852** | **1,742,393** |
| Biashara na Matengenezo | 449,262 | 472,657 | 538,900 | 562,425 | 560,887 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 244,611 | 266,921 | 292,806 | 306,218 | 344,112 |
| Huduma za Malazi na Chakula | 85,324 | 91,339 | 101,000 | 102,719 | 114,656 |
| Habari na Mawasiliano | 59,339 | 63,284 | 67,821 | 71,176 | 71,797 |
| Fedha na Bima | 164,403 | 191,678 | 177,568 | 176,237 | 176,233 |
| Upangishaji Majengo | 116,197 | 133,952 | 133,575 | 155,042 | 167,679 |
| Shughuli za Kitaalamu, Sayansi na Ufundi | 20,318 | 22,479 | 26,928 | 29,866 | 32,304 |
| Utawala na ulinzi | 19,349 | 20,931 | 18,698 | 21,391 | 19,576 |
| Elimu | 124,134 | 126,843 | 128,032 | 124,739 | 140,556 |
| Afya na Huduma za Jamii | 46,427 | 51,316 | 57,333 | 64,128 | 73,809 |
| Huduma Nyingine | 25,340 | 30,239 | 35,559 | 37,910 | 40,787 |
| **Jumla ya Pato la Mkoa** | **3,743,015** | **4,039,088** | **4,753,275** | **5,022,780** | **5,418,844** |

**Chanzo:** NBS na Ofisi ya Mkuu wa Mko wa Dodoma

**Jedwali la 5: Pato la Mkoa kwa shughuli za kiuchumi kwa Halmashauri, (Bei ya Mwaka Husika), 2018**

**Shilingi Milioni**

| Shughuli za Uchumi/Halmashauri | Kondoa | Mpwapwa | Kongwa | Chamwino | Dodoma Jiji | Bahi | Chemba | Kondoa Mji | Pato la Mkoa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kilimo** | **325,333** | **141,310** | **170,017** | **126,558** | **158,621** | **274,819** | **145,193** | **18,762** | **1,360,612** |
| Mazao | 300,826 | 111,172 | 141,189 | 89,000 | 116,327 | 254,182 | 123,936 | 13,338 | 1,149,969 |
| Mifugo | 23,794 | 28,473 | 28,811 | 30,647 | 40,545 | 20,407 | 21,204 | 5,393 | 199,275 |
| Misitu na Uwindaji | 178 | 1,665 | 16 | 4,443 | 605 | 149 | 53 | 31 | 7,140 |
| Uvuvi | 535 | 0 | 0 | 2,468 | 1,144 | 81 | 0 | 0 | 4,228 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **35,433** | **70,569** | **86,066** | **59,656** | **496,998** | **150,370** | **22,827** | **105,778** | **1,027,697** |
| Uchimbaji madini na mawe | 14,765 | 17,924 | 22,137 | 19,292 | 24,689 | 126,748 | 13,348 | 3,395 | 242,298 |
| Utengenezaji bidhaa | 8,480 | 22,501 | 25,280 | 15,984 | 184,765 | 9,247 | 3,700 | 43,984 | 313,940 |
| Umeme | 833 | 2,211 | 2,484 | 1,570 | 18,152 | 908 | 364 | 4,321 | 30,842 |
| Maji | 495 | 1,505 | 1,473 | 1,036 | 12,369 | 605 | 269 | 2,416 | 20,168 |
| Ujenzi | 10,860 | 26,429 | 34,693 | 21,774 | 257,023 | 12,861 | 5,146 | 51,663 | 420,448 |
| **Huduma** | **78,745** | **131,305** | **145,537** | **129,197** | **580,334** | **97,262** | **73,598** | **118,729** | **1,354,707** |
| Biashara na Matengenezo | 43,116 | 57,992 | 66,680 | 70,420 | 104,320 | 47,564 | 48,187 | 10,983 | 449,262 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 6,607 | 17,532 | 19,697 | 12,454 | 143,963 | 7,205 | 2,883 | 34,270 | 244,611 |
| Huduma za Malazi na Chakula | 2,305 | 6,115 | 6,871 | 4,344 | 50,216 | 2,513 | 1,006 | 11,954 | 85,324 |
| Habari na Mawasiliano | 1,603 | 4,253 | 4,778 | 3,021 | 34,923 | 1,748 | 699 | 8,314 | 59,339 |
| Fedha na Bima | 3,994 | 10,598 | 11,907 | 7,528 | 100,023 | 4,355 | 1,743 | 24,256 | 164,403 |
| Upangishaji Majengo | 3,139 | 8,328 | 9,357 | 5,916 | 68,387 | 3,423 | 1,370 | 16,279 | 116,197 |
| Shughuli za Kitaalamu, Sayansi na Ufundi | 594 | 1,311 | 1,673 | 1,100 | 12,324 | 539 | 216 | 2,562 | 20,318 |
| Utawala na ulinzi | 3,153 | 1,829 | 1,309 | 1,786 | 4,602 | 4,545 | 1,502 | 623 | 19,349 |
| Elimu | 9,429 | 11,849 | 14,879 | 14,586 | 38,023 | 20,129 | 11,023 | 4,216 | 124,134 |
| Afya na Huduma za Jamii | 4,122 | 9,683 | 6,346 | 6,751 | 8,639 | 4,495 | 4,671 | 1,721 | 46,427 |
| Huduma Nyingine | 684 | 1,816 | 2,041 | 1,290 | 14,914 | 746 | 299 | 3,550 | 25,340 |
| **Pato la Mkoa** | **439,511** | **343,183** | **401,620** | **315,411** | **1,235,953** | **522,450** | **241,618** | **243,269** | **3,743,015** |

**Jedwali la 6: Pato la Mkoa kwa shughuli za kiuchumi kwa Halmashauri, (Bei ya Mwaka Husika), 2019**

**Shilingi Milioni**

| Shughuli za Uchumi/Halmashauri | Kondoa | Mpwapwa | Kongwa | Chamwino | Dodoma Jiji | Bahi | Chemba | Kondoa Mji | Pato la Mkoa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kilimo** | **333,827** | **172,620** | **218,291** | **139,376** | **173,747** | **198,160** | **160,799** | **25,317** | **1,422,136** |
| Mazao | 312,472 | 139,234 | 184,276 | 96,116 | 124,043 | 173,800 | 135,592 | 18,864 | 1,184,396 |
| Mifugo | 20,943 | 31,705 | 33,992 | 35,902 | 47,677 | 24,014 | 25,136 | 6,422 | 225,791 |
| Misitu na Uwindaji | 153 | 1,681 | 23 | 5,222 | 793 | 171 | 71 | 31 | 8,145 |
| Uvuvi | 260 | 0 | 0 | 2,136 | 1,233 | 175 | 0 | 0 | 3,804 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **39,138** | **87,839** | **93,317** | **69,139** | **538,146** | **163,993** | **28,248** | **125,492** | **1,145,312** |
| Uchimbaji madini na mawe | 15,913 | 24,091 | 24,394 | 25,764 | 33,250 | 138,748 | 18,038 | 4,609 | 284,808 |
| Utengenezaji bidhaa | 10,009 | 26,427 | 29,711 | 18,653 | 217,444 | 10,839 | 4,370 | 52,181 | 369,635 |
| Umeme | 499 | 1,318 | 1,481 | 930 | 10,842 | 540 | 218 | 2,602 | 18,430 |
| Maji | 634 | 4,104 | 1,867 | 1,276 | 14,137 | 781 | 348 | 3,113 | 26,260 |
| Ujenzi | 12,082 | 31,900 | 35,864 | 22,515 | 262,473 | 13,084 | 5,275 | 62,987 | 446,180 |
| **Huduma** | **83,134** | **149,891** | **156,001** | **135,906** | **633,568** | **101,355** | **77,367** | **134,418** | **1,471,639** |
| Biashara na Matengenezo | 44,420 | 67,247 | 68,092 | 71,918 | 109,660 | 48,104 | 50,351 | 12,865 | 472,657 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 7,212 | 19,636 | 21,407 | 13,440 | 156,671 | 7,810 | 3,148 | 37,597 | 266,921 |
| Huduma za Malazi na Chakula | 2,473 | 6,530 | 7,342 | 4,609 | 53,732 | 2,678 | 1,080 | 12,894 | 91,339 |
| Habari na Mawasiliano | 1,714 | 4,524 | 5,087 | 3,193 | 37,228 | 1,856 | 748 | 8,934 | 63,284 |
| Fedha na Bima | 5,190 | 13,704 | 15,407 | 9,673 | 112,758 | 5,621 | 2,266 | 27,059 | 191,678 |
| Upangishaji Majengo | 3,627 | 9,577 | 10,767 | 6,760 | 78,799 | 3,928 | 1,584 | 18,910 | 133,952 |
| Shughuli za Kitaalamu, Sayansi na Ufundi | 609 | 1,607 | 1,807 | 1,134 | 13,224 | 659 | 266 | 3,173 | 22,479 |
| Utawala na ulinzi | 3,011 | 1,829 | 1,370 | 2,137 | 4,812 | 4,588 | 1,595 | 1,589 | 20,931 |
| Elimu | 9,433 | 12,806 | 15,200 | 14,027 | 39,230 | 20,214 | 10,729 | 5,205 | 126,843 |
| Afya na Huduma za Jamii | 4,626 | 10,269 | 7,091 | 7,489 | 9,666 | 5,010 | 5,244 | 1,922 | 51,316 |
| Huduma Nyingine | 819 | 2,162 | 2,431 | 1,526 | 17,789 | 887 | 357 | 4,269 | 30,239 |
| **Pato la Mkoa** | **456,099** | **410,351** | **467,609** | **344,421** | **1,345,460** | **463,508** | **266,414** | **285,227** | **4,039,088** |

**Chanzo:** NBS na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

**Jedwali la 7: Pato la Mkoa kwa shughuli za kiuchumi kwa Halmashauri, (Bei ya Mwaka Husika), 2020**

**Shilingi Milioni**

| Shughuli za Uchumi/ Halmashauri | Kondoa | Mpwapwa | Kongwa | Chamwino | Dodoma Jiji | Bahi | Chemba | Kondoa Mji | Pato la Mkoa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kilimo** | **381,599** | **147,153** | **381,286** | **164,184** | **209,910** | **382,204** | **177,751** | **29,872** | **1,873,958** |
| Mazao | 359,609 | 112,677 | 348,059 | 119,731 | 155,828 | 356,347 | 151,459 | 22,716 | 1,626,426 |
| Mifugo | 21,750 | 32,764 | 33,199 | 36,992 | 52,214 | 24,854 | 26,207 | 7,123 | 235,103 |
| Misitu na Uwindaji | 178 | 1,712 | 28 | 5,823 | 744 | 290 | 85 | 32 | 8,892 |
| Uvuvi | 61 | 0 | 0 | 1,638 | 1,124 | 713 | 0 | 0 | 3,537 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **42,595** | **94,185** | **114,197** | **74,694** | **615,642** | **186,085** | **29,786** | **143,911** | **1,301,096** |
| Uchimbaji madini na mawe | 15,980 | 24,071 | 36,010 | 25,579 | 37,072 | 157,371 | 18,121 | 4,652 | 318,855 |
| Utengenezaji bidhaa | 10,993 | 28,880 | 32,491 | 20,253 | 238,102 | 11,823 | 4,801 | 57,601 | 404,943 |
| Umeme | 421 | 1,106 | 776 | 776 | 9,121 | 453 | 184 | 2,207 | 15,044 |
| Maji | 614 | 1,806 | 1,807 | 1,212 | 15,399 | 751 | 310 | 3,019 | 24,918 |
| Ujenzi | 14,587 | 38,321 | 43,114 | 26,875 | 315,948 | 15,688 | 6,371 | 76,433 | 537,336 |
| **Huduma** | **91,680** | **164,576** | **169,872** | **148,979** | **665,665** | **109,408** | **86,202** | **141,839** | **1,578,221** |
| Biashara na Matengenezo | 51,457 | 77,514 | 78,542 | 82,367 | 120,347 | 55,341 | 58,353 | 14,979 | 538,900 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 7,949 | 20,882 | 23,493 | 14,645 | 172,167 | 8,549 | 3,472 | 41,650 | 292,806 |
| Huduma za Malazi na Chakula | 2,742 | 7,203 | 8,104 | 5,052 | 59,387 | 2,949 | 1,197 | 14,367 | 101,000 |
| Habari na Mawasiliano | 1,841 | 4,837 | 5,442 | 3,392 | 39,878 | 1,980 | 804 | 9,647 | 67,821 |
| Fedha na Bima | 4,820 | 12,664 | 14,247 | 8,881 | 104,408 | 5,184 | 2,105 | 25,258 | 177,568 |
| Upangishaji Majengo | 3,626 | 9,526 | 10,718 | 6,681 | 78,541 | 3,900 | 1,584 | 19,000 | 133,575 |
| Shughuli za Kitaalamu, Sayansi na Ufundi | 731 | 1,921 | 2,162 | 1,347 | 15,828 | 787 | 319 | 3,832 | 26,928 |
| Utawala na ulinzi | 3,024 | 1,829 | 1,340 | 2,303 | 3,593 | 4,396 | 1,413 | 800 | 18,698 |
| Elimu | 9,363 | 13,820 | 15,095 | 14,273 | 39,857 | 19,735 | 10,680 | 5,210 | 128,032 |
| Afya na Huduma za Jamii | 5,161 | 11,844 | 7,877 | 8,261 | 10,751 | 5,550 | 5,852 | 2,037 | 57,333 |
| Huduma Nyingine | 965 | 2,536 | 2,853 | 1,778 | 20,908 | 1,038 | 422 | 5,058 | 35,559 |
| **Pato la Mkoa** | **515,873** | **405,915** | **665,355** | **387,858** | **1,491,216** | **677,698** | **293,739** | **315,621** | **4,753,275** |

**Chanzo:** NBS na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

**Jedwali la 8: Pato la Mkoa kwa shughuli za kiuchumi kwa Halmashauri, (Bei ya Mwaka Husika), 2021**

**Shilingi Milioni**

| Shughuli za Uchumi/ Halmashauri | Kondoa | Mpwapwa | Kongwa | Chamwino | Dodoma Jiji | Bahi | Chemba | Kondoa Mji | Pato la Mkoa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kilimo** | **381,536** | **173,905** | **309,210** | **282,941** | **232,065** | **319,416** | **176,445** | **31,741** | **1,907,259** |
| Mazao | 360,426 | 136,816 | 272,831 | 235,868 | 168,520 | 289,898 | 147,538 | 24,291 | 1,636,189 |
| Mifugo | 20,920 | 35,838 | 36,337 | 40,203 | 61,157 | 27,133 | 28,820 | 7,433 | 257,840 |
| Misitu na Uwindaji | 155 | 1,252 | 42 | 5,905 | 1,016 | 186 | 87 | 17 | 8,660 |
| Uvuvi | 34 | 0 | 0 | 965 | 1,372 | 2,199 | 0 | 0 | 4,571 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **47,186** | **109,294** | **125,540** | **86,720** | **696,913** | **197,208** | **35,884** | **164,924** | **1,463,669** |
| Uchimbaji madini na mawe | 16,942 | 29,891 | 37,107 | 31,559 | 42,299 | 164,832 | 22,624 | 5,835 | 351,088 |
| Utengenezaji bidhaa | 12,431 | 32,495 | 36,583 | 22,643 | 268,446 | 13,277 | 5,431 | 65,466 | 456,771 |
| Umeme | 438 | 1,288 | 797 | 797 | 9,451 | 467 | 191 | 2,305 | 15,734 |
| Maji | 646 | 1,887 | 1,818 | 1,247 | 15,433 | 763 | 329 | 3,213 | 25,337 |
| Ujenzi | 16,729 | 43,733 | 49,235 | 30,474 | 361,284 | 17,868 | 7,310 | 88,106 | 614,739 |
| **Huduma** | **96,010** | **177,061** | **178,405** | **154,599** | **692,825** | **112,942** | **90,381** | **149,629** | **1,651,852** |
| Biashara na Matengenezo | 53,663 | 80,436 | 81,558 | 84,926 | 127,943 | 57,317 | 60,880 | 15,701 | 562,425 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 8,333 | 21,784 | 24,525 | 15,180 | 179,966 | 8,901 | 3,641 | 43,888 | 306,218 |
| Huduma za Malazi na Chakula | 2,795 | 7,307 | 8,227 | 5,092 | 60,368 | 2,986 | 1,221 | 14,722 | 102,719 |
| Habari na Mawasiliano | 1,937 | 5,063 | 5,701 | 3,528 | 41,831 | 2,069 | 846 | 10,201 | 71,176 |
| Fedha na Bima | 4,796 | 12,538 | 14,115 | 8,736 | 103,575 | 5,123 | 2,096 | 25,259 | 176,237 |
| Upangishaji Majengo | 4,219 | 11,030 | 12,417 | 7,686 | 91,119 | 4,507 | 1,844 | 22,221 | 155,042 |
| Shughuli za Kitaalamu, Sayansi na Ufundi | 813 | 2,125 | 2,392 | 1,481 | 17,552 | 868 | 355 | 4,280 | 29,866 |
| Utawala na ulinzi | 2,988 | 1,829 | 1,386 | 2,594 | 6,031 | 4,552 | 1,423 | 589 | 21,391 |
| Elimu | 9,935 | 15,819 | 16,691 | 14,796 | 30,740 | 19,646 | 11,387 | 5,725 | 124,739 |
| Afya na Huduma za Jamii | 5,498 | 16,433 | 8,356 | 8,701 | 11,420 | 5,873 | 6,238 | 1,609 | 64,128 |
| Huduma Nyingine | 1,032 | 2,697 | 3,036 | 1,879 | 22,280 | 1,102 | 451 | 5,433 | 37,910 |
| **Jumla ya Pato la Mkoa** | **524,732** | **460,260** | **613,155** | **524,260** | **1,621,803** | **629,566** | **302,711** | **346,294** | **5,022,780** |

**Chanzo:** NBS na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

**Jedwali la 9: Pato la Mkoa kwa shughuli za kiuchumi kwa Halmashauri, (Bei ya Mwaka Husika), 2022**

Shilingi Milioni

| Shughuli za Uchumi/ Halmashauri | Kondoa | Mpwapwa | Kongwa | Chamwino | Dodoma Jiji | Bahi | Chemba | Kondoa Mji | Pato la Mkoa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kilimo** | **408,092** | **190,156** | **359,147** | **303,162** | **303,370** | **374,898** | **186,130** | **33,403** | **2,158,358** |
| Mazao | 384,944 | 151,025 | 317,382 | 249,327 | 229,725 | 344,738 | 154,138 | 25,810 | 1,857,090 |
| Mifugo | 23,010 | 37,895 | 41,713 | 45,689 | 71,487 | 28,626 | 31,889 | 7,560 | 287,868 |
| Misitu na Uwindaji | 109 | 1,236 | 52 | 7,567 | 913 | 150 | 103 | 34 | 10,164 |
| Uvuvi | 28 | 0 | 0 | 579 | 1,245 | 1,384 | 0 | 0 | 3,236 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **43,352** | **102,946** | **131,401** | **93,576** | **727,214** | **210,527** | **38,298** | **170,779** | **1,518,093** |
| Uchimbaji madini na mawe | 17,842 | 29,384 | 42,584 | 35,427 | 55,757 | 176,981 | 24,727 | 5,862 | 388,563 |
| Utengenezaji bidhaa | 10,206 | 29,313 | 35,826 | 23,325 | 276,335 | 13,443 | 5,447 | 69,905 | 463,801 |
| Umeme | 359 | 1,261 | 821 | 821 | 11,673 | 473 | 192 | 2,125 | 17,725 |
| Maji | 657 | 1,951 | 2,015 | 1,349 | 19,220 | 809 | 306 | 3,395 | 29,702 |
| Ujenzi | 14,288 | 41,037 | 50,155 | 32,654 | 364,229 | 18,820 | 7,626 | 89,493 | 618,302 |
| **Huduma** | **85,596** | **172,498** | **180,639** | **163,624** | **783,437** | **117,766** | **93,130** | **145,702** | **1,742,393** |
| Biashara na Matengenezo | 45,467 | 74,879 | 82,422 | 90,279 | 130,000 | 59,890 | 63,011 | 14,938 | 560,887 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 6,893 | 19,797 | 24,196 | 15,753 | 223,954 | 9,079 | 3,679 | 40,761 | 344,112 |
| Huduma za Malazi na Chakula | 2,856 | 7,494 | 8,570 | 5,928 | 70,064 | 2,840 | 1,151 | 15,752 | 114,656 |
| Habari na Mawasiliano | 1,970 | 5,123 | 5,161 | 3,360 | 42,768 | 1,937 | 785 | 10,694 | 71,797 |
| Fedha na Bima | 3,530 | 10,139 | 12,392 | 8,068 | 114,695 | 4,650 | 1,884 | 20,875 | 176,233 |
| Upangishaji Majengo | 4,240 | 12,178 | 14,884 | 9,690 | 93,764 | 5,585 | 2,263 | 25,074 | 167,679 |
| Shughuli za Kitaalamu, Sayansi na Ufundi | 647 | 1,858 | 2,271 | 1,479 | 21,024 | 852 | 345 | 3,826 | 32,304 |
| Utawala na ulinzi | 3,309 | 1,829 | 1,515 | 2,038 | 3,973 | 4,645 | 1,576 | 690 | 19,576 |
| Elimu | 11,090 | 15,831 | 17,702 | 15,678 | 41,723 | 20,920 | 11,380 | 6,232 | 140,556 |
| Afya na Huduma za Jamii | 4,777 | 21,022 | 8,659 | 9,484 | 14,927 | 6,292 | 6,620 | 2,029 | 73,809 |
| Huduma Nyingine | 817 | 2,347 | 2,868 | 1,867 | 26,545 | 1,076 | 436 | 4,831 | 40,787 |
| **Jumla ya Pato la Mkoa** | **537,040** | **465,600** | **671,188** | **560,361** | **1,814,020** | **703,191** | **317,559** | **349,885** | **5,418,844** |

**Chanzo:** NBS na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

**Jedwali la 10: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi kwa Halmashauri kwa Bei ya Mwaka Husika kwa , 2022**

Asilimia

| Shughuli za Kiuchumi/ Halmashauri | Kondoa | Mpwapwa | Kongwa | Chamwino | Dodoma Jiji | Bahi | Chemba | Kondoa Mji | Pato la Mkoa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kilimo** | **7.5** | **3.5** | **6.6** | **5.6** | **5.6** | **6.9** | **3.4** | **0.6** | **39.8** |
| Mazao | 7.1 | 2.8 | 5.9 | 4.6 | 4.2 | 6.4 | 2.8 | 0.5 | 34.3 |
| Mifugo | 0.4 | 0.7 | 0.8 | 0.8 | 1.3 | 0.5 | 0.6 | 0.1 | 5.3 |
| Misitu na Uwindaji | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.2 |
| Uvuvi | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.1 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **0.8** | **1.9** | **2.4** | **1.7** | **13.4** | **3.9** | **0.7** | **3.2** | **28.0** |
| Uchimbaji madini na mawe | 0.3 | 0.5 | 0.8 | 0.7 | 1.0 | 3.3 | 0.5 | 0.1 | 7.2 |
| Utengenezaji bidhaa | 0.2 | 0.5 | 0.7 | 0.4 | 5.1 | 0.2 | 0.1 | 1.3 | 8.6 |
| Umeme | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.2 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.3 |
| Maji | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.4 | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 0.5 |
| Ujenzi | 0.3 | 0.8 | 0.9 | 0.6 | 6.7 | 0.3 | 0.1 | 1.7 | 11.4 |
| **Huduma** | **1.6** | **3.2** | **3.3** | **3.0** | **14.5** | **2.2** | **1.7** | **2.7** | **32.2** |
| Biashara na Matengenezo | 0.8 | 1.4 | 1.5 | 1.7 | 2.4 | 1.1 | 1.2 | 0.3 | 10.4 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 0.1 | 0.4 | 0.4 | 0.3 | 4.1 | 0.2 | 0.1 | 0.8 | 6.4 |
| Huduma za Malazi na Chakula | 0.1 | 0.1 | 0.2 | 0.1 | 1.3 | 0.1 | 0.0 | 0.3 | 2.1 |
| Habari na Mawasiliano | 0.0 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.8 | 0.0 | 0.0 | 0.2 | 1.3 |
| Fedha na Bima | 0.1 | 0.2 | 0.2 | 0.1 | 2.1 | 0.1 | 0.0 | 0.4 | 3.3 |
| Upangishaji Majengo | 0.1 | 0.2 | 0.3 | 0.2 | 1.7 | 0.1 | 0.0 | 0.5 | 3.1 |
| Shughuli za Kitaalamu, Sayansi na Ufundi | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.4 | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 0.6 |
| Utawala na ulinzi | 0.1 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 0.1 | 0.0 | 0.0 | 0.4 |
| Elimu | 0.2 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.8 | 0.4 | 0.2 | 0.1 | 2.6 |
| Afya na Huduma za Jamii | 0.1 | 0.4 | 0.2 | 0.2 | 0.3 | 0.1 | 0.1 | 0.0 | 1.4 |
| Huduma Nyingine | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.5 | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 0.8 |
| **Jumla ya Pato la Mkoa** | **9.9** | **8.6** | **12.4** | **10.3** | **33.5** | **13.0** | **5.9** | **6.5** | **100.0** |

**Chanzo:** NBS na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

**Jedwali la 11: Vyanzo vya Taarifa zilizotumika kutayarisha Pato la Mkoa kwa Shughuli ya kiuchumi**

| No | Shughuli za kiuchumi | Vyanzo vya taarifa |
|---|---|---|
| 1 | Kilimo | Mazao: Maafisa kilimo na Maafisa ugani |
| | | Misitu: Maliasili |
| | | Mifugo: Maafisa Mifugo |
| | | Uvuvu: Idara ya Uvuvi |
| 2 | Uchimbaji Madini na Mawe | Ofisi ya Madini ya Mkoa |
| 3 | Utengenezaji bidhaa | Viwanda |
| 4 | Umeme | TANESCO na Taasisi nyingine zinazolisha umeme |
| 5 | Maji safi na Maji taka | Mamlaka za Maji Mijini/Vijijini |
| 6 | Ujenzi | Serikali za Mitaa, Makampuni ya Ujenzi yaliochaguliwa, ikiwa ni pamoja na TANROADS na Kampuni Binafsi |
| 7 | Biashara za Jumla na Rejareja | Wauzaji wa Jumla na Wafanyabiashara wa Rejareja Waliochaguliwa |
| 8 | Usafirishaji Mizigo | Waendeshaji wa vyombo vya usafiri waliochaguliwa wa Anga/Reli/Barabara (Umma na Binafsi) |
| 9 | Huduma za Malazi na Chakula | Huduma za Malazi na Chakula |
| 10 | Habari na Mawasiliano | Huduma za Posta na Mawasiliano ya simu (Umma na Binafsi) |
| 11 | Fedha na Bima | Benki, Maduka ya kubadilishia fedha, Madalali, Makampuni ya Bima, Taasisi za Fedha na Vyama vya Mikopo |
| 12 | UpangishajiMajengo | Nyumba za Kupangisha zilizochzguliwa, Serikali ya Mtaa |
| 13 | Shughuli za Kitaalamu, Sayansi na Ufundi | Wahasibu/Wakaguzi Waliochaguliwa, Wanasheria, Washauri, nk |
| 14 | Utawala na Ulinzi | Serikali za Mitaa, Hazina Ndogo |
| 15 | Elimu | Watoa Huduma za Elimu Waliochaguliwa (Serikali na Binafsi) |
| 16 | Afya na Huduma za Jamii | Watoa Huduma za Afya waliochaguliwa (Serikali na Binafsi) |
| 17 | Huduma Nyingine | Saluni za Wasusi/Vinyozi, Vilabu vya Michezo, Watengeneza saa, Mafundi Viatu/ Ukarabati n.k. |

**Chanzo:** NBS na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

## Rejea


1. United Nations New York (2009)*: The System of National accounts2008.* *https://unstats.un.org/unsd/nationalaccount/docs/SNA2008.pdf*
2. United Nations New York (2008): International Standard Industrial *Classification of All Economic Activities Revision 4* *https://unstats.un.org/unsd/publication/seriesM/seriesm_4rev4e.pdf*


Kondoa
Chemba
Dodoma
Urban
Kongwa
Bahi
Mpwapwa
Chamwino